WANAMUZIKI MASHUHURI WAKO HAPO MOMBASA

WANAMUZIKI MASHUHURI wa Osibisa kutoka Uingereza wanatarajiwa kuwafumbuiza mashabaki wao hapa mjini hapo kesho Jumamosi kuanzia saa moja na nusu usiku hadi saa nne katika uwanja wa Munispaa Mombasa. Tikiti zapatikana sehemu zote mjini.

WANAONEKANA wanafunzi wa Hudaa Muslim School na walimu wao.

HUDAA MUSLIM SCHOOL YAFUNGULIWA

BAADA ya kazi iliyoendelea kadiri ya mwaka mzima, sasa Hudaa Muslim School imefunguliwa na Madrasa hii, ni aina ya kipekee Kenya nzima ambayo imegharimu kiasi cha shillingi 328,167.95 mpaka kumalizika.

Kwa wakati mmoja, inaweza kuchukua wanafunzi hata mia nne, na juu pia ina uwanja wa nafasi kama hiyo pindi ikitokea dharau ya kufanya hivyo.

Katika mkutano wake wa kukabidhi jengo hilo kwa wazazi na kuanzisha masomo mara moja, paliochaguliwa kamati ya kuendesha madarasa hiyo, na pia kukubaliana katika mambo fulani kama vile sasa karo itakuwa shillingi saba baada ya tano kila mwezi ili shillingi mbili zilipio maji na moto wa umeme, mambo ambayo hayakuzingatiwa hapo mbeleni.

Mwalimu mkuu wa madrasa hiyo alisema kwamba mlango wa Madrasa utakuwa wazi kuanzia saa kumi na mbili asubuhi mpaka kufikia saa nne za usiku, na walimu wenye harara ya kusomesha watakaa hapo chonjo kungojea wanafunzi.

Aliongeza kwamba elimu nyingine za fani mbali mbali zitakuwa zikifundishwa hapo kwa watu wazima na kwa walimu wenyewe pia. Maalim hakusahau kukumbusha kwamba kanzu na kofia zitakuwa muhimu kuvaliwa hasa siku mwisho wa wiki.

Kamati mpya ni: mwenyekiti Bw. Abdulaziz Mohammed; mwandishi, Maalim Omar Islam (mwalimu mkuu); mshika hazina, Bw. Juma Ali; katibu mtendaji, Bw. Ashur Jumaan, na wanachama Alhaji Salim, Moh'd Matano na Abdurahman Hassani.

TWAOBOLEZA KIFO CHA GUNDA

Msiba kwetu msiba
Nyoyo zinachoma miba
Kwa kifo cha wetu baba
Mungu akulaze pema

Machozi kwa milizamu
Zimetutoka fahamu
Khatima ya mwanadamu
Mungu amlaze pema

Kwanza tasifu elimu
Na lugha akikalimu
Leo etwa marehemu
Mungu amlaze pema

Mwalimu wa waalimu
Darasani ni timamu
Aliye mtaalamu
Mungu amlaze pema

Toka kwao huko Vanga
Aliwafanya wamanga
Si hoja kwake upanga
Mungu amlaze pema

Pengo hili ni kabiru
Msiba umekithiru
Machoni hamuna nuru
Mungu amlaze pema

Msiba kwa madirasa
Zimepotea furusa
Pia kwa wanasiasa
Mungu amlaze pema

Tabia zake halua
Kila aliyemjua
Leo ametushitua
Mungu amlaze pema

Msiba vipembe vyote
Hutamuona ye yote
Kibuhuti chetu sote
Mungu amlaze pema

Subira twaomba kwako
Sisi ni watumwa wako
Ufalume wote wako
Mungu akulaze pema

Pwani umetungilia
Sote tumejinamia
Shekhe Ali tunalia
Marehemu Ali Gunda.

Machoni yametwenea
Twenda tukipindukia
Mwisho taaga dunia
Marehemu Ali Gunda.

Mungu kambarikia
Mwarabu atakimbia
Dunia ametwachia
Marehemu Ali Gunda.

Kilinge alipasua
Hakuna asomjua
Mungu amemchukua
Marehemu Ali Gunda.

Hata Bara kasambaa
Mbele yake kushangaa
Vitabu vilizagaa
Marehemu Ali Gunda.

Haliwezi kujazika
Ni shida kuelezeka
Twapita tukianguka
Marehemu Ali Gunda.

Na baitu talibina
Elimu kila namna
Menyaji hawana tena
Marehemu Ali Gunda.

Hakujua kujivuna
Atakiri muungwana
Kamuondosha Rabana
Marehemu Ali Gunda.

Watu wote walizana
Mzee au kijana
Tuauni Maulana,
Marehemu Ali Gunda.

Muumba wetu jalia
Utuwene tukilia
Huna wakukungilia
Marehemu Ali Gunda.

MAALIM BURHANI (Bahari Mbasi), SERANI, MOMBASA.

Futeni majina ya kikabila

TWAMPONGEZA RAIS Moi kwa hatua nyingine thabiti aliyochukua ya kupiga vita ukabila katika mchezo wa mpira. Hii ni hatua ifaayo katika wakati mzuri ambapo viongozi wengi wamo njiani kukomesha vyama vyenye majina ya ukabila.

Nchini Kenya kuna michezo aina aina kwani raia wa nchi hii ni wanamichezo waliojitokeza ulimwenguni kote kwa ubingwa wao. Kwa mfano, kuna chama cha Mabondia, Chama cha Wapiganaji myereka, chama cha Judo, chamca cha Taikondo, na chama cha Riadha kwa ujumla.

Majina ya vyama hivi vikitajwa, ndani yake hakuna ishara hata ndogo ya ukabila, kwani katika michezo, hiyo yote yachezwa ni makabila yote, bila ya ubaguzi, kitu muhimu ni ule ubingwa wa mtu. Jambo hili ni la raha sana, kwa vile mwana riadha akitaka kujiunga na klabu fulani, hana haja ya kukaa kwanza akafikiria ile kabila yake.

Kenya kuna timu za mpira kama: Luo Union, Abaluhya, Maragoli, Kisumu Hot Stars, Gema, Ugenya, Digo United, Bukusu, Luanda na kadhalika. Timu hizi ukisikia majina yao tu, utajua ni kabila gani ambazo sana zimehusika na kuziongoza.

Na hatusemi kwamba, kwa mfano katika timu ya Luo, huwa wanaoshiriki ni Wajaluo watupu. La. Kwa mujibu wa Rais wetu, ni kwamba majina haya hayana maana. Na ni bora majina yatayoleta umoja na udugu wa nchi nzima kuliko kukusanya kabila moja pekee.

Hii ndiyo sababu Rais wetu apendaye umoja na upendano, akapendekeza kwamba iundwe timu moja ya Taifa na iitwe 'Nyayo II'! Na kwa kufuata maongozi haya ya Nyayo, viongozi wa timu za kandanda, wanaweza wakaanzisha utaratibu wa kutoa timu moja ya taifa ya kuwakilisha Mkoa mzima katika mashindano ya Ligi ya kila mwaka.

Mkoa wa Nairobi unaweza kutoa hata timu mbili au tatu zenye majina ya kitaifa nazo zikashiriki. Maoni ya watu mbali mbali yanasema kwamba utaratibu huu, unaweza ukaleta matatizo ya kifedha lakini wanaamini kwamba kutapungua chuki za kikabila.

Na sisi twasema kwamba hata ikiwa pesa zitaleta mzozo iwapo watu watapendana ndilo jambo muhimu, na haya ndiyo maongozi ya Nyayo.

HII NI timu ya Mpira wa kikapu (netball) kutoka Mombasa High School, wanaonekana pamoja na mwalimu Mkuu wa skuli hiyo pamoja na walimu wengine.

WASICHANA WAWILI waliovalia maridadi, Bi Naazlin Haji (kushoto) na Bi Rosemary Thomas wakiwa Severin Sea Lodge wakati wa mkutano wa kimataifa ulio tayarishwa na Pan African Insurance Co. Ltd Mombasa. PICHA: NATIONAL STUDIO

SAUTI ZA WASOMAJI

COASTWEEK Sanduku La Posta 87270 Mombasa KENYA

TWATAKA ARIDHI

IDHAA ya Sauti ya Kenya ilitangaza katika Television kwamba ombi la wakazi wa Shimoni kutaka kumiliki ardhi litachunguzwa vyema na Serikali.

Bwana S. Ngelechi aliuhakikishia ujumbe huo uliongozwa na Diwani Rashid Mrafi kuwa ni wale wenyeji halisi ndio wanaoweza kudai (kuomba) kumiliki aridhi.

Serikali ya Kenya inaangalia na Kulinda haki za wananchi wote hata wengineo ambao ni wageni wanaoingiza fedha au rasili mali zao kutoka nchi za kigeni. Haki ni haki lazima ilindwe.

Bwana ngelechi ni afisa wa Serikali ya Nyayo naye hana budi kuwasaidia wananchi wanaostahili kupewa vipande vya ardhi.

Jambo muhimu inambidi asishawishiwe kwenda kinyume cha sheria za nchi pamoja na kuvunja katiba ya Kenya.

Wakazi wa Shimoni si maskwata peke yao ambao ni Wenyeji, hata wengine wanahitajia kupatiwa ardhi kama sehemu zao wanamoishi.

Pia baadhi yao ni wenyeji wa asili walio na haki kila upande kuendelea kudumu katika aridhi hizo.

Serikali iko macho kulinda haki ya kila mmoja bila ubaguzi au mapendeleo.

A. Saggaf Alawy, MOMBASA.

Coastweek ★★

SWAHILI CROSSWORD NO. 102

JEMBE
UNGA SAFI NO. 1



KWENDA KULIA:
1. Makusudio
6. Jenga
7. Kufanya kuwa na nguvu
9. ET haigeuki
10. Ndani kwa Kimombo
11. Kunguwaa
12. Kitongoji pande za Lamu
14. Kataa
15. Namna ya ndege
16. Aina ya mti wa maua

KWENDA CHINI:
1. Mtukutu
2. Vipele vidogo vinavyoletwa na joto
3. Asali
4. Yamtama
5. Sinyaa, kuwa nyonge
8. Apenda
12. Kutia paa la nyumba kabla ya kuezeka
13. Funguo nyingi zilizo pamoja
15. Taabani

JINA.

SANDUKI LA POSTA

Washindi wa Fumbo la Kujaza Maneno No. 100

[1] R. M. Karrabu, P.O. Kinango, via Mombasa,

[2] Hussein Abdalla Idha, Sanduku la Posta 82367, Mombasa,

[3] Hussein Salim Charo, Sanduku la Posta 90491, Mombasa.

Washindi waombwa wafike afisini mwa *COASTWEEK*

MAJIBU YA SHINDANO LA FUMBO LA KUJAZA MANENO NO. 100 —

KWENDA KULIA:
1. NYANGUMI, 6. TONE, 7. AMBARI, 8. AM, 10. UFUGAJI 14. LAKINI, 15. KIUA, 17. MBIZI, 18. SHINA.

KWENDA CHINI:
1. NGAMUA, 2. NYANGAU, 3. UTIAJI, 4. MO, 5. INDA, 9. MH, 11. ULIMI, 12. AKAMA 13. INDIA, 16. PIA.

Shindano la Fumbo la Kujaza Maneno:

Uamuzi wa majaji utakuwa wa mwisho. Hakuna malalamiko yoyote yatakayokubaliwa.

Washindo watatu wa kwanza kila mmoja atapatiwa 'T'-shirt moja ya Jembe.

Shindano hili limedhaminiwa na *COASTWEEK LTD* pamoja na ATTA LTD, Mombasa.

Jawabu za fumbo hili lipelekwe kwa Muhariri, *COASTWEEK*, Sanduku la Posta 87270, Mombasa, Kenya. Siku ya Alhamisi tarehe 13.11.80 saa sita mchana shindano hili litakuwa mwisho.